# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Posta,
S.L.P. 2599,
33101 MWANZA,
Barua Pepe: rbcmwanza@pccb.go.tz.
www.pccb.go.tz

**MWANZA – JULAI 22, 2020**

## TAARIFA KWA UMMA
## KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

## TAKUKURU MWANZA YAOKOA ZAIDI YA SHILINGI MILIONI 53 NA KUSHINDA KESI 18 KATIKA KIPINDI CHA APRILI - JUNI, 2020

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza imefanikiwa kuokoa **Sh. 53,086,720/=** katika kipindi cha mwezi Aprili - Juni, 2020.

Kati ya fedha hizo kiasi cha **Sh. 8,325,420/=** zimewekwa kwenye akaunti maalum ya Serikali iliyopo Benki Kuu; Sh. 24,377,300/= zimerejeshwa kwa wahusika vikiwemo Vyama vya Ushirika na watu binafsi na kiasi cha Sh. 20,384,000/= zitakabidhiwa kwa viongozi wa Kata ya Nyamhongolo.

Fedha hizi **20,384,000/=** zilikuwa zimefanyiwa ubadhirifu kwenye mradi wa MORAM wa mtaa wa Bupumula Kata ya Nyamhongolo Manispaa ya Ilemela ambapo Mwenyekiti wa Mtaa huo Bw. MARCO MARTIN NCHEYE alifanya ubadhirifu wa fedha za mauzo ya MORAM kwa kuziweka kwenye akaunti yake na kuzitumia kwa matumizi yake binafsi.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Mwanza ulibaini kwamba, malipo ya manunuzi ya MORAM yalifanywa na kampuni ya STECO LTD ambayo inajenga kituo kipya cha mabasi ya abiria katika kata ya Nyamhongolo Manispaa ya Ilemela na baada ya TAKUKURU kufanya uchunguzi imeweza kudhibiti upotevu wa fedha hizo na tayari mhusika amezirejesha. Fedha hizi zitakabidhiwa kwa viongozi wa Kata ya Nyamhongolo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo wenye manufaa kwa wananchi.

Pia katika kipindi cha Aprili – Juni 2020, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imeshinda kesi 18 kati ya kesi 21 zilizotolewa maamuzi ambapo jumla ya washtakiwa 18 walitiwa hatiani. Aidha majalada 28 yamechunguzwa na kukamilika na kesi mpya 23 zimefunguliwa Mahakamani.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi hicho TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imepokea jumla ya taarifa 227 za malalamiko mbalimbali yakiwemo ya vitendo vya rushwa.

Takwimu zinaonesha kuwa Serikali za Mitaa zinaongoza kwa kulalamikiwa. Kati ya taarifa zilizopokelewa, taarifa 54 zinahusu serikali za mitaa (Wenyeviti na watendaji wa vijiji, mitaa, vitongoji na kata), ikifuatiwa na idara ya Elimu malalamiko 23, Polisi 20, Taasisi za fedha 17, vyama vya Siasa 14, Mahakama 12, Ardhi 10, Vyama vya ushirka 10, Uvuvi 7, Afya 6, Kilimo 5, Biashara 3, Mamlaka ya bandari Tanzania 3, Mifuko ya hifadhi ya jamii 2, Ujenzi 2, Maji 2, Misitu 2, Maendeleo ya jamii 2, Utawala 2, kampuni za ulinzi 2, Mifugo 1, Ustawi wa jamii 1, RITA 1, Mazingira 1, NIDA 1, TRA 1, Maliasili (TANAPA) 1 na Sekta Binafsi 22.

**Uzuaiji Rushwa**

Katika kuhakikisha kwamba fedha za Serikali zinadhibitiwa na kufanya lengo lililokusudiwa, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza katika kipindi cha mwezi Aprili - Juni 2020, imefanya ukaguzi wa miradi 14 ya maendeleo yenye thamani ya **Sh. 4,306,214,092/=**.

Kati ya miradi hiyo 14 iliyokaguliwa, miradi 6 ni ya Elimu ambayo ina thamani ya **Sh. 557,000,000/=,** miradi 4 ya Afya yenye thamani ya **Sh 1,356,000,000/=** , miradi 3 ni ya ujenzi wa mitaro na ukarabati wa Barabara ambayo ina thamani ya **Sh. 159,695,110 /=** na mradi 1 wa Maji wenye thamani ya **Sh 2,233,518,982 /=.**

**Hata hivyo,** mradi 1 umekutwa na kasoro ambapo hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa mradi haiendani na thamani ya fedha iliyotumika, hivyo uchunguzi kuhusiana na mradi huo umeanzishwa.

Mradi huo ni wa ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Misungwi wenye thamani ya **Sh. 56,000,000/=** .

Pamoja na ukaguzi wa miradi hiyo, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imefanya uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa. Chambuzi zilizofanywa, ni za mfumo wa manunuzi ya umma kupitia Force Account, uendeshaji na usimamizi wa vyama vya ushirika katika Halmashauri ya jiji la Mwanza, mianya ya rushwa katika ugawaji wa pembejeo za kilimo cha zao la pamba katika Halmashauri ya jiji la Mwanza pamoja na mfumo wa utendaji kazi wa Watendaji wa Vijiji na Kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa.

## Elimu kwa Umma

Kwa upande wa elimu kwa umma katika kipindi cha Aprili – Juni, 2020 TAKUKURU Ofisi ya Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya jiji la Mwanza pamoja na Ofisi ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa pamoja tumeweza kutoa semina kwa viongozi wote wa Serikali za Mitaa kwenye Kata zote 18 za Wilaya ya Nyamagana.

Semina hiyo elekezi ilihusu majukumu ya viongozi hao na mipaka yao ya kazi, makatazo ya rushwa pamoja na umuhimu wa kuzingatia maadili wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Viongozi wa Serikali za Mitaa walioelimishwa ni Wenyeviti wa Mitaa, Wajumbe pamoja na Watendaji wa Mitaa na Kata.

Aidha TAKUKURU imeweka mkakati wa kuwaelimisha Viongozi wa Serikali za Vijiji na Mitaa kwa Mkoa mzima wa Mwanza kwani ni vipindi vinne sasa mfululizo imeonekana Serikali za Mitaa kuongoza kwa kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa.

Ni matumaini yetu kuwa baada ya viongozi hao kupatiwa elimu tunataraji kuwe na mabadiliko chanya kwa kupunguza malalamiko ya vitendo vya rushwa kwenye Serikali za Mitaa.

Katika kipindi cha Aprili - Juni, 2020 - TAKUKURU imeweza kuyafikia makundi mbalimbali na kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa kufanya Mikutano ya hadhara 12, Semina 25, Vipindi 3 vya redio, kushiriki kwenye Maonesho 2, Uandishi wa habari na makala 14 na kuimarisha klabu 64 za wapinga rushwa kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo.

Aidha, TAKUKURU mkoa wa Mwanza itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na katika kipindi cha Julai - Septemba 2020 TAKUKURU Mkoa wa Mwanza itajikita zaidi kuelimisha wananchi kuhusu makatazo ya rushwa kwenye uchaguzi na kwa yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya rushwa atakamatwa na atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

**Wito kwa Wananchi;**

Nawakumbusha wananchi wa mkoa wa Mwanza kwamba kipindi cha mchakato wa uchaguzi sio kipindi cha mavuno, ambacho wananchi wanaweza kukitumia kujipatia chochote kwa njia za rushwa. Badala yake ni kipindi cha wananchi kutafakari kuhusu changamoto walizonazo na viongozi sahihi wa kutatua changamoto hizo.

Rushwa ya kiwango chochote itakayotolewa na mgombea yeyote, inaweza kuwagharimu wananchi kwa kukosa maendeleo na kutokuwa na utatuzi wa changamoto zinazozunguka maisha yao ya kila siku kwa kipindi cha miaka mitano au maisha yao yote. Hii ni kwa sababu mgombea akichaguliwa kwa kutoa rushwa, atajikita zaidi katika kurejesha fedha alizotumia kutoa hongo wakati wa uchaguzi na hatajali maendeleo ya wananchi.

Tuchague viongozi wazalendo, waadilifu na wachapakazi watakaoleta maendeleo katika maeneo yetu na si kuchagua viongozi kwa misingi ya rushwa.

***KATAA RUSHWA, JENGA TANZANIA***

**"Kwa taarifa za vitendo vya rushwa tumia TAKUKURU APP, piga simu ya dharura namba 113 au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au Piga *113# fuata maelekezo" Huduma hii ni ya BURE.**

**IMETOLEWA NA:**

……………………….

**EMMANUEL STENGA**

**MKUU WA TAKUKURU (M) MWANZA**